



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI

TAARIFA KWA UMMA

Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilipokea barua kutoka kwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye kwa kuzingatia kifungu cha 37(3) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, ameitaarifu Tume kuwepo kwa nafasi wazi ya Ubunge katika Jimbo la Liwale Mkoa wa Lindi, kuanzia tarehe 13 Agosti, 2018, kufuatia aliyekuwa Mbunge wa Jimbo hilo Ndugu Zuberi Mohamed Kuchauka kujiuzulu uanachama wa Chama cha Wananchi - CUF, na hivyo kupoteza sifa ya kuwa Mbunge.

Aidha, kwa mujibu wa vifungu vya 37 (1) (b),(5) na 46 (2) vya Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Tume inatoa taarifa kwa Umma kuwa Jimbo la **Liwale** lipo wazi na Uchaguzi huo utafanyika kwa ratiba ifuatayo:-

- 1. Kutoa Fomu za Uteuzi itakuwa kati ya tarehe 07 hadi 13 Septemba mwaka huu.**
- 2. Uteuzi wa Wagombea utafanyika tarehe 13 Septemba mwaka huu.**
- 3. Kampeni za Uchaguzi zitaanza tarehe 14 Septemba na kumalizika tarehe 12 Oktoba mwaka huu.**
- 4. Siku ya Uchaguzi itakuwa tarehe 13 Oktoba mwaka huu.**

Tume inavikumbusha Vyama vya Siasa na wadau wote wa Uchaguzi kuzingatia Sheria, Kanuni, Maadili ya Uchaguzi, Miongozo, na Maelekezo yote wakati wa kipindi cha Uchaguzi huo Mdogo.

Imetolewa leo tarehe 24 Agosti, 2018 na;

Jaji (R) Semistocles S. Kaijage

MWENYEKITI

TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI